



**TANZANIA INSURANCE
REGULATORY AUTHORITY**

**TAKAFUL OPERATIONAL
GUIDELINES**

APRIL, 2022

Version No.1.0@2022

**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA
TANZANIA**

**MWONGOZO WA UENDESHAJI WA
TAKAFUL**

APRILI, 2022

Toleo No. 1.0@2022

CONTENTS	YALIYOMO
SECTION ONE: INTRODUCTION.....1	SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI..... 1
SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS.....10	SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA.....10
SECTION THREE: ESTABLISHMENT OF MAINTENANCE OF TAKAFUL FUND.....23	SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL23
SECTION FOUR: REGISTRATION OF TAKAFUL INSURANCE COMPANY34	SEHEMU YA NNE: USAJILI WA KAMPUNI YA BIMA YA TAKAFUL..... 34
SECTION FIVE: DEFICIT AND LOSS RECTIFICATION POLICY.....35	SEHEMU YA TANO: SERA YA UREKEBISHAJI WA NAKISI NA HASARA.....35
SECTION SIX: PRODUCT.....38	SEHEMU YA SITA: BIDHAA.....38
SECTION SEVEN: UNDERWRITING OF TAKAFUL RISKS.....47	SEHEMU YA SABA: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL.....47
SECTION EIGHT: CLAIMS MANAGEMENT.....52	SEHEMU YA NANE: USIMAMIZI WA MADAI.....52
SECTION NINE: INVESTMENT OF TAKAFUL FUNDS.....53	SEHEMU YA TISA: UWEKEZAJI WA FEDHA ZA TAKAFUL.....53
SECTION TEN: SURRENDER OF CERTIFICATES.....56	SEHEMU YA KUMI: KUKABIDHI HATI.....56
SECTION ELEVEN: RIGHTS AND OBLIGATIONS OF THE PARTICIPANT.....58	SEHEMU YA KUMI NA MOJA: HAKI NA MAJUKUMU YA MSHIRIKI.....58
SECTION TWELVE: ESTABLISHMENT OF AN OPERATING MODEL.....60	SEHEMU YA KUMI NA MBILI: KUTENGENEZA MUUNDO WA UENDESHAJI.....60

SECTION THIRTEEN: GOVERNANCE OF THE TAKAFUL OPERATOR.....	70	SEHEMU YA KUMI NA TATU: UTAWALA WA MUENDESHA TAKAFUL.....	70
SECTION FOURTEEN: RE-TAKAFUL.....	82	SEHEMU YA KUMI NA NNE: TAKAFUL MTAWANYO	82
SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES.....	83	SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO WA KIHASIBU.....	83
SECTION SIXTEEN: DISSOLUTION OF THE TAKAFUL OPERATOR.....	103	SEHEMU YA KUMI NA SITA: KUFUTWA KWA MUENDESHA TAKAFUL.....	103
SCHEDULES.....	104	SCHEDULES	104

SECTION ONE: INTRODUCTION		SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI	
1.1 Authorization and Powers	1.1.1 These Insurance (Takaful) Guidelines 2022 are issued under Section 5 (2) and 11(a - e) of the Insurance Act Cap 394	1.1 Idhini na Mamlaka	1.1.1 Mwongozo huu ya Bima ya Takaful ya Mwaka 2022 imetolewa chini ya idhini ya vifungu 5(2) na 11 (a-e) vya Sheria ya Bima Sura Na. 394
1.2 Citation	These Guidelines may be cited as “ <i>Takaful Guidelines, 2022</i> ”	1.2 Nukuu	Mwongozo huu itafahamika kama “ <i>Mwongozo wa Takaful, 2022</i> ”
1.3 Application	1.3.1. These guidelines shall apply to all entities licensed to conduct Takaful businesses undertakings and all other matters related thereto. 1.3.2. The Takaful operators shall be required to adhere to the existing regulatory	1.3 Matumizi	1.3.1. Mwongozo huu utahusu taasisi zote zenye leseni ya kuendesha biashara za bima ya Takaful na shughuli zingine zozote zinazowiana na Takaful. 1.3.2. Waendeshaji wa Bima ya Takaful watatakiwa kuzingatia

	<p>requirements in addition to fulfilling the specific provisions for Takaful operations as laid out in these Guidelines.</p>		<p>masharti ya udhibiti wa huduma za bima yaliyowekwa pamoja na kutimiza maelekezo mahususi ya uendeshaji wa Takaful kama ilivyoainishwa katika Mwongozo huu.</p>
<p>1.4. Background and Rationale</p>	<p>1.4.1 These Guidelines seek to address the market need of increasing the distribution, penetration, employment and availability of insurance services. In response to this need, the Authority held a number of consultative stakeholder meetings to obtain their views and suggestions and conducted research, hence preparation of these Takaful Guidelines.</p>	<p>1.4. Usuli na Mantiki</p>	<p>1.4.1 Mwongozo huu umetokana na hitaji la soko la kuongeza usambazaji, wigo, ajira na upatikanaji wa huduma za bima. Ili kukidhi hitaji hilo Mamlaka ilifanya mikutano na wadau wa bima kwa nyakati tofauti ili kupokea maoni na mapendekezo na utafiti na hatimaye Mwongozo huu wa Takaful ukaandaliwa.</p> <p>1.4.2 Takaful ni mfumo wa Bima ambao unajumuisha vipengele vya kuchangiana na kushirikiana, miamala ya kimaadili, bila kujali imani na mafungamano ya mtu.</p>

	1.4.2 Takaful is a form of insurance which incorporates elements of mutuality, ethical finance considerations and is open to all people regardless of faith and background		
1.5 Purpose and Objectives	1.5.1. The purpose is to increase penetration and contribution of insurance subsector to the Gross Domestic Product (GDP).	1.5 Lengo na Madhumuni	1.5 .1Lengo ni kuongeza wigo na mchango wa bima katika pato la taifa
	1.5.2. To establish a mechanism of regulating and supervising the Takaful business undertakings.		1.4.1 Kuweka mfumo wa kudhibiti na kusimamia biashara na shughuli za bima ya Takaful.
	1.4.1 Provide a framework for investment of Takaful funds.		1.4.2 Kuweka mfumo wa uwekezaji wa fedha za bima ya Takaful.
	1.4.2 Set requirements and minimum standards for		1.4.3 Kuweka vigezo na viwango katika uendeshaji na udhihirishaji unaolenga kulinda masilahi ya watumiaji/washiriki.

	<p>operation and disclosure that aims to protect the interests of consumers/participants.</p> <p>1.4.3 Promote and support professional development of the Takaful business undertakings.</p> <p>1.4.4 These Guidelines are issued to provide operational guidance for the Takaful business undertakings in Tanzania</p>		<p>1.4.4 Kuhamasisha na kuchochea ukuaji wa utaalumu wa biashara na miamala ya bima ya Takaful.</p> <p>1.4.5 Madhumuni ya Mwongozo huu ni kutoa mwongozo wa usimamizi na udhibiti wa shughuli za biashara ya bima ya Takaful nchini</p>
<p>1.6 Scope of Applicability</p>	<p>1.5.1 These Guidelines cover all operations relating to Takaful business including;</p> <p>a. Establishment of Takaful-operating models.</p>	<p>1.5 Wigo wa Matumizi</p>	<p>1.5.1 Mwongozo huu unajumuisha mambo yote ya uendeshaji yanayohusu biashara ya Takaful ikiwemo:</p> <p>(a) Kuweka miundo ya uendeshaji wa bima ya Takaful.</p>

	<p>b. Setting specific governance standards for the Takaful business</p> <p>c. Takaful fund management methods</p> <p>d. Management of Takaful participants (policyholders)</p> <p>1.5.2 Operator's specific operational requirements As to matters not provided for herein, relevant provisions in the Insurance Act, Regulations, instruments and directives issued by the Commissioner shall apply, provided that the referred provision does not</p>		<p>(b) Kuweka masharti maalum ya uendeshaji na usimamizi wa biashara ya bima ya Takaful</p> <p>(c) Njia za usimamizi wa mfuko wa bima ya Takaful.</p> <p>(d) Usimamizi wa washiriki wa huduma ya bima ya Takaful</p> <p>1.5.2 Mahitaji mahususi ya kiuendeshaji kwa wasimamizi wa bima ya Takaful. Kwa masuala ambayo hayakutajwa kwenye Mwongozo huu, vifungu husika katika sheria ya Bima, kanuni, Mwongozo utakaotolewa na Kamishna wa Bima utatumika, pale ambapo kifungu tajwa hakikinzani na misingi ya sheria za Kiislamu.</p> <p>1.5.3 Ikitokea vifungu tajwa hapo juu vinakinzana na misingi ya sheria za Kiislamu, Kamishna atajulishwa</p>
--	--	--	---

	<p>contravene Shariah principles.</p> <p>1.5.3 Where the provisions indicated above contravene the Shariah principles, the Commissioner shall be notified accordingly for further guidance.</p>		<p>ipasavyo kwa ajili ya kutoa muongozo.</p>
<p>1.7 Definitions</p>	<p>1.6.1 The following terms have been used in these Guidelines and shall be deemed to denote the following meanings herein:</p> <p>“Board” refers to the board of directors of a Takaful operator.</p> <p>“Family Takaful” refers to the act of providing insurance protection to Takaful Participants and/or beneficiaries in the event of illness,</p>	<p>1.6 Maana ya Maneno</p>	<p>1.6.1 Istilahi zifuatazo zimetumika katika Mwongozo huu kuelezea maana zilizokusudiwa kama ifuatavyo:</p> <p>“Bodi” inakusudia bodi ya wakurugenzi wa taasisi endeshaji Takaful</p> <p>“Takaful ya Familia” ina maanisha kitendo cha kuweka kinga ya bima kwa washiriki wa Takaful na/au wanufaika kwa ajili ya ugonjwa, kifo au ulemavu wa jumla wa mwili wa kudumu au mwisho wa mkataba.</p> <p>“Mwenye sifa Zinazotakiwa” anakusudiwa mtu anayonekana kwa</p>

	<p>death or total permanent disability or at the end of the policy.</p> <p>“Fit and Proper” refers to a person who, on the basis of documents and evidence available is honest, trustworthy, fair, possessing integrity and ability to make sound and effective decisions in his/her activities and has requisite skills and experience for conducting the intended activities.</p> <p>“General Takaful” refers to insurance for the protection of participants against losses arising from specified perils other than family Takaful.</p> <p>“Mudaraba based Takaful contract” means a Takaful contract based on profit sharing ratio among Takaful Participants themselves and</p>		<p>msingi ya nyaraka na Ushahidi kuwa ni mkweli, muaminifu, mtenda haki, muadilifu na mwenye uwezo wa kufanya maamuzi ya busara na yenye manufaa katika shughuli zake na ana stadi zinazotakiwa na uzoefu wa kutekeleza majukumu yake yaliyokusudiwa.</p> <p>“Takaful ya Kawaida” inamaanisha bima ya kuwakinga washiriki dhidi ya hasara zinazotokana na majanga yaliyoainishwa tofauti na yale ya Takaful ya familia.</p> <p>“Mkataba wa Takaful kwa msingi wa Mudharaba” unamaanisha mkataba wa Takaful wenye msingi wa kugawana kiwango cha faida miongoni mwa washiriki wa Takaful na Muendeshaji pamoja na kinga dhidi ya majanga kwa washiriki wa Takaful.</p>
--	--	--	---

	<p>between Takaful participants and the Operator together with the provision of risks cover to Takaful participants.</p> <p>“Operating model” refers to a model that defines the relationship and fiduciary duties between the Takaful operator and the participants.</p> <p>“Participant” (policyholder/contributor) means the party contributing to the Takaful fund that is covered through the mutual protection and solidarity of the Takaful contract.</p> <p>“Participants documents” means the documents detailing the benefits and obligations of a Participant under a Takaful Contract</p> <p>“Takaful Participants Investment</p>	<p>“Muundo wa Uendeshaji” Inamaanisha uhusiano na majukumu ya kuaminiwa baina ya Muendesha Takaful na washiriki.</p> <p>“Mshiriki” (mwenye mkataba /mchangiaji) inamaanisha mhusika anayechangia kwenye mfuko wa Takaful na anakingwa kwa kinga jumuishi na mshikamano kupitia mkataba wa Takaful.</p> <p>“Nyaraka za washiriki” ni nyaraka zenye taarifa za mafao na wajibu wa mshiriki kwa mnasaba wa Mkataba wa Takaful.</p> <p>“Mfuko wa uwekezaji wa Washiriki wa Takaful” ni mfuko kutokana na fedha kutoka kwenye mfuko wa washiriki wa Takaful wenye lengo la kuwekeza au kuweka akiba, na hii ni mahsusi kwa Takaful ya familia tu.</p> <p>“Mfuko wa tahadhari ya majanga kwa Washiriki” (Mfuko wa Majanga) ni mfuko ulioundwa kutokana na sehemu ya</p>
--	---	--

	<p>Fund” refers to a fund from the Takaful Participants Fund for the purpose of investment or savings and applies to only family Takaful.</p> <p>“Participants Risk Fund” refers to a Takaful Fund established to pool a portion of Takaful participant’s contributions for the purpose of meeting Takaful claims associated with events or risks specified in the Takaful contract.</p> <p>“Re-Takaful” means an arrangement consistent with sound principles of Takaful for covering risks managed by the Operator in the course of carrying on Takaful Business and includes ceding risks from Participant Takaful Funds managed by the Operator(s) to one or more Re-Takaful pool(s).</p>	<p>michango ya Washiriki wa Takaful kwa lengo la kukidhi madai ya Takaful yanayoambatana na matukio au majanga yaliyoanishwa katika mkataba wa Takaful.</p> <p>“Takaful Mtawanyo” ni utaratibu unaowiana na misingi thabiti ya misingi ya Takaful kwa ajili ya kuinga majanga yanayo simamiwa na waendeshaji wa Takaful katika shughuli zao na inajumuisha kuhawilisha majanga kutoka kwenye Mifuko ya Washiriki wa Takaful inayosimamiwa na Muendeshaji/Waendeshaji kwenda kwenye Takaful Mtawanyo moja au zaidi.</p> <p>“Mfuko wa Takaful” ni mkusanyo wa fedha inayochangiwa na Washiriki kwa lengo la kusaidiana panapotokea majanga.</p> <p>“Mkopo wa hisani (Qardh Hasana)” ni mkopo usio na riba unaotolewa na Muendeshaji Takaful kwenda kwenye</p>
--	--	--

	<p>“Takaful fund” refers to a pool of money that participants contribute to help each other in case of a risk.</p> <p>“Benevolent loan (Qardh Hasana)” refers to an interest free loan granted by the Takaful operator to the participants’ risk fund in the event of a deficit;</p> <p>“Shariah Board” refers to a Board of Shariah scholars formed within a Takaful company to provide Shariah opinions on the transactions, conducts of the company and their conformity with the Shariah rules and principles.</p> <p>“Shari’ah compliant investment” means investment which complies with Shariah rules and principles.</p>	<p>Mfuko wa Majanga wa washiriki panapotokea nakisi.</p> <p>“Bodi ya Shariah” ni Bodi ya wanazuoni wa Sheria za Kiislamu iliyoundwa ndani ya kampuni ya Takaful ili kutoa Mwongozo, hukumu na maelekezo kwa mujibu wa kanuni na misingi ya Shariah kuhusu miamala na mwenendo wa uendeshaji wa kampuni husika na kukidhi kwake kanuni na misingi ya Shariah.</p> <p>“Uwekezaji unaoafikiana na Sharia” ni uwekezaji unaofuata kanuni na misingi ya Shariah.</p> <p>“Mfuko wa Wanahisa” ni akaunti ya mtaji inayotunza mtaji uliochangiwa na wanahisa wa kampuni ya Takaful.</p> <p>“Takaful” ni mfumo wenye kuwiana na matakwa ya Sharia wenye lengo la kufikia ushirikiano baina ya washiriki wa Takaful ili kusaidiana wakati wa majanga mahususi</p>
--	--	---

<p>“Shareholders’ Fund” refers to the account that holds the paid up capital provided by the company’s shareholders.</p> <p>“Takaful” refers to a Shariah compliant contractual system aiming at attaining cooperation between a group of participants to cover specific risks whereby each participant pays a certain contribution that leads to formation of the Takaful Fund.</p> <p>“Takaful Operator ” means an entity or a person authorized to carry on Takaful business in Tanzania.</p> <p>“Takaful benefits” includes any benefit, whether pecuniary or otherwise, which is secured by a Takaful Contract.</p> <p>“TIRA” denotes Tanzania Insurance Regulatory Authority.</p>	<p>ambapo kila mshiriki anachangia kiasi fulani cha fedha kwenye mfuko wa Takaful.</p> <p>“Muendeshaji wa Takaful” ni taasisi au mtu aliyeidhinishwa kuendesha biashara ya Takaful nchini.</p> <p>“Mafao ya Takaful” ni mafao yote yaliyomo ndani ya Mkataba wa Takaful, yawe ya kipesa au mengineyo.</p> <p>“TIRA” inamaanisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania</p> <p>“Sera ya Kutathmini Majanga na Kiwango cha Michango” ni sera inayotumika kuamua kiwango cha majanga yatakayobebwa na Mfuko wa Takaful dhidi ya michango ya washiriki.</p> <p>“Mkataba wa Uwakala” ni mkataba wa Takaful kwa misingi ya Uwakala katika uendeshaji wa biashara ya bima ya Takaful.</p> <p>“Mkataba wa Wakfu” ni mkataba wa Takaful kwa misingi ya Wakfu kama kitendo</p>
--	---

	<p>“Underwriting policy” means policy used to determine the extent of risk acceptance of Takaful risk fund against payment of contribution.</p> <p>“Wakala based contract” means a Takaful contract based on the contract of agency.</p> <p>“Waqf based contract” means a Takaful contract based on Islamic endowment rules for a specified purpose</p> <p>“Mutual indemnification” means the cooperative and collaborative element of Takaful where the participants mutually provide insurance cover for one another in the event of any risk.</p> <p>“Tabarru” means a donation, charity or gift.</p>	<p>cha ihsani kwa lengo maalumu.(katika uendeshaji wa Takaful) .</p> <p>“Fidia Jumuishi” ni ushirikiano wa washiriki wa Takaful ambapo kila mshiriki anachangia malipo ya bima kwa ajili ya kujilinda na janga lolote litapotokea kwa pamoja.</p> <p>“Tabarru” ni mchango, msaada au zawadi.</p> <p>“Mtaji wa tabaka la kwanza” ni mtaji wa msingi uliopo katika kanzi za Muendesha huduma za Takaful na hutumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za kibiashara. Hii ni pamoja na hisa za kawaida, bakaa ya faida na bakaa zingine.</p> <p>“Mtaji wa tabaka la pili” ni tabaka la ziada la mtaji wa Muendeshaji wa Takaful na unajumuisha bakaa ya tathmini ya mali ya mali zisizohamishika, <i>nyenzo mseto za kifedha, Sukuk, na mikataba ya madeni</i></p>
--	---	--

	<p>“Tier 1 capital” refers to the core capital held by the Takaful operator and is used to fund business activities. It includes ordinary shares, as well as disclosed reserves and other reserves.</p> <p>“Tier 2 capital” means a designated second or supplementary layer of Takaful operator's capital and is composed of items such as revaluation reserves, hybrid instruments, and subordinated term debt.</p>		<p><i>yanayopaswa kulipwa kabla ya madeni mengine.</i></p>
1.8 Takaful Concept	<p>1.7.1 Takaful is an insurance system through which the participants donate part or all of their contributions, under the management of Takaful Operator whose role is to manage the operations, pay</p>	1.8 Nadharia ya Takaful	<p>1.7.1 Takaful ni mfumo wa bima ambao washiriki hutoa sehemu au michango yao yote chini ya usimamizi wa Muendeshaji ambaye kazi yake ni kusimamia shughuli za uendeshaji, kulipa fidia na kuwekeza kwa misingi ya Shariah.</p>

	<p>claims and invest the contributions in line with Shariah principles.</p> <p>1.7.2 Takaful is based on two principles:</p> <p>(a) Co-operative system: a group facing a common risk forms a collective pool which takes collective responsibility for that risk. The collective (or common) pool is owned by its members or participants.</p> <p>(b) Tabarru – these are donations made by participants to the Takaful pool for the purpose of compensating pool members who suffered a</p>		<p>1.7.2 Takaful imejengwa juu ya misingi miwili:</p> <p>(a) Mfumo wa Ushirika: kundi ambalo limeunda mfuko jumuishi wa kukabiliana na majanga kwa kushirikiana. Mfuko jumuishi unamilikiwa na wanachama au washiriki wote.</p> <p>(b) Tabarru – Michango inayotolewa na washiriki wa Mfuko wa Takaful kwa ajili ya kuwafidia waathirika wa majanga pale yanapotokea.</p>
--	---	--	---

	loss due to a risk covered by the pool.		
--	---	--	--

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
2.1 Operational Framework	2.1.1 A Takaful operator carrying Takaful business has the duty to manage the Takaful operations in accordance with Shariah and in the best interest of the Takaful participants. This includes operating the business in a sound and prudent manner.	2.1 Miongozo wa Utendaji	2.1.1 Muendesha wa biashara ya Takaful anawajibika kuendesha shughuli hizo katika misingi ya Shariah na kwa ajili ya maslahi ya washiriki. Hii ni pamoja na kuendesha biashara akizingatia umahiri na weledi.
	2.1.2 The Board of Directors, Chief Executive Officer, the management team and their relevant committees of Takaful Operator shall be responsible for the implementation of Shariah Board's decisions.		2.1.2 Bodi ya Wakurugenzi, Afisa Mtendaji Mkuu na Uongozi wa kampuni pamoja na kamati zao za uendeshaji Takaful watakuwa na wajibu wa kutekeleza maamuzi ya Bodi ya Shariah.
	2.1.3 The management must ensure that the Shariah contracts and Shariah matters		2.1.3 Uongozi wa kampuni unawajibika kuhakikisha kuwa Mikataba ya Shariah na masuala ya Shariah yanayohusiana na mfumo wa uendeshaji

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<p>in relation to the operational framework are endorsed by the Shariah board at all times.</p> <p>2.1.4 The management must ensure that the operational framework is commensurate with the nature and complexity of the Takaful business and considers the types of funds being managed and relevant Shariah contracts adopted in managing the Takaful business. In this regard, the operational framework must include, at the minimum, policies and procedures on:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Application of Shariah contracts; (b) Establishment and maintenance of Takaful and shareholders funds (c) Product structuring; 		<p>yanaidhinishwa na Bodi ya Shariah wakati wote.</p> <p>2.1.4 Uongozi wa kampuni unawajibika kuhakikisha kuwa mfumo wa uendeshaji unaendana na mazingira ya biashara ya Takaful na inazingatia aina za mifuko inayosimamiwa na mikataba husika na inatiliwa maanani katika kusimamia biashara ya Takaful. Kwa muktadha huu, mfumo wa uendeshaji ni lazima, kwa uchache uwe na sera na taratibu za:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Utekelezaji wa mikataba ya Shariah (b) Kuanzisha na kuendeleza mifuko ya Takaful na ya Wanahisa. (c) Muundo wa bidhaa

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<ul style="list-style-type: none"> (d) Management of underwriting; (e) Management of re-Takaful; (f) Management of investments; (g) Management of claims; (h) Remuneration for management of Takaful funds; (i) Management of surplus (j) Management of deficiency and loss rectification. (k) The method for calculation of investment profit for participants' investment fund (l) Any other relevant information required for understanding of the operating model. 		<ul style="list-style-type: none"> (d) Usimamizi wa kufanya tathmini ya majanga na kiwango cha michango. (e) Usimamizi wa bima mtawanyo za Takaful (f) Usimamizi wa vitega uchumi(uekezaji) (g) Usimamizi wa madai (h) Malipo kwa ajili ya usimamizi wa mifuko ya Takaful (i) Usimamizi wa ziada itokanayo baada ya kulipa fidia (j) Usimamizi wa mapungufu wa mfuko wa Takaful (k) Utaratibu wa kukotoa faida ya mfuko wa uwekezaji kwa washiriki. (l) Taarifa nyingine yeyote itakayohitajika ili kuelewa muundo wa uendeshaji.
2.1.5	The management shall be responsible to ensure effective implementation of	2.1.5	Uongozi wa kampuni utawajibika kuhakikisha kwamba kuna utekelezaji

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<p>the operational framework which includes having in place;</p> <p>(a) Adequate Information Technology Systems for Takaful business.</p> <p>(b) Adequate human resources with relevant competencies;</p> <p>(c) Appropriate internal controls system; and</p> <p>(d) Clear communication plan of the policies and procedures to personnel involved in the day-to-day management of Takaful operations</p> <p>(e) Clear policy for security and adequacy of systems.</p> <p>(f) Provide clear terms of reference regarding the Shariah board's mandate and responsibilities.</p> <p>(g) Well defined operating procedures and reporting lines of the Shariah Board</p>		<p>madhubuti wa mfumo wa uendeshaji ambao ni pamoja na kuwepo;</p> <p>(a) Mifumo ya Teknolojia ya Habari yenye kutosheleza kwa biashara ya Takaful</p> <p>(b) Rasilimaliwatu ya kutosha yenye elimu na stadi muafaka</p> <p>(c) Mifumo mwafaka ya udhibiti</p> <p>(d) Mpango wa mawasiliano unaoelewika wa sera na taratibu kwa wafanyakazi wanaohusika na utendaji wa kila siku katika usimamizi wa shughuli za biashara ya Takaful</p> <p>(e) Sera bayana ya usalama na kujitosheleza kwa mifumo</p> <p>(f) Kuweka bayana hadidi za rejea kuhusu mamlaka na majukumu ya Bodi ya Shariah.</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS	SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA
<p>(h) To support Shariah board by appointing head of internal Shariah compliance whereby the Shariah board will be able to mandate and delegate some of its functions.</p> <p>2.1.6 The following aspects of training shall be taken into consideration</p> <p>(a) The Commissioner may prescribe any special training or qualification for any particular designation.</p> <p>(b) The Takaful Operators, intermediaries and service providers shall provide sufficient and relevant training to all its staff.</p> <p>(c) For the purposes of the foregoing provision, the operators, intermediaries and service providers may arrange an in-</p>	<p>(g) Kuwa na taratibu zilizowazi za uendeshaji na mfumo wa kupeana taarifa wa Bodi ya Shariah.</p> <p>(h) Kuisaidia Bodi ya Shariah kumteua Mkuu wa Kitengo cha Shariah. Bodi ya Shariah inaweza kukaimisha baadhi ya majukumu yake kwa Mkuu wa Kitengo.</p> <p>2.1.6 Vipengele vya mafunzo vifuatavyo vitazingatiwa:</p> <p>(a) Kamishna anaweza akaagiza mafunzo maalum au vigezo vyovyote kwa nafasi yoyote ile.</p> <p>(b) Waendeshaji wa Takaful, watu wa kati na watoa huduma watawajibika kutoa mafunzo ya Takaful ya kutosha na mwafaka kwa wafanyakazi wao wote.</p> <p>(c) Kwa madhumuni ya kifungu hicho hapo juu, waendeshaji, watu wa kati na watoa</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<p>house training or train their staff through institutions that provide this training recognized by the Authority.</p> <p>2.1.7 The Takaful Operators, intermediaries and service providers shall manage their operations in compliance with the Shariah and in line with their articles of association (memorandum and articles).</p> <p>2.1.8 The management shall review the operational model on a regular basis in response to changes in the business and operating environment in line with the international best practices. Any change(s) on the operational model shall be subject to prior approval by the Shariah board and Commissioner</p>		<p>huduma wanaweza wakaandaa mafunzo katika vituo vya kazi au kuwapa mafunzo wafanyakazi wao kupitia taasisi zinazotambuliwa na Mamlaka.</p> <p>2.1.7 Waendeshaaji, watu wa kati na watoa huduma wa Takaful watasimamia uendeshaaji wa shughuli zao katika misingi ya Shariah na kwa mujibu wa katiba za Kampuni zao.</p> <p>2.1.8 Uongozi wa kampuni utapaswa kupitia muundo wa utendaji mara kwa mara kuendana na mabadiliko ya kibiashara na mazingira ya utendaji kwa kuzingatia viwango bora vya kimataifa. Mabadiliko yeyote ndani ya muundo wa utendaji yanapaswa kupata idhini ya Bodi ya Shariah na Kamishna.</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
<p>2.2 Conditions Applicable to Operator</p>	<p>2.2.1 Takaful operator:</p> <p>(a) Shall ensure that the Principal Officer of a Takaful Operator possesses qualifications and experience relevant to Takaful Business</p> <p>(b) Shall appoint a Shariah compliance officer in accordance with the provisions of these guidelines</p> <p>(c) Shall ensure that Family Takaful business is divided into sub-funds including Participant Takaful Funds, Participant Investment Funds and any other Funds as guided by the Shariah board and as advised by the appointed actuary;</p> <p>(d) Carrying out General Takaful business shall set up one or more Participant Takaful Funds and an Operator Fund.</p>	<p>2.2 Masharti Yanayowa husu Waendesh aji</p>	<p>2.2.1 Muendesha Takaful:</p> <p>(a) Atalazimika kuwa na Afisa Muendesha mwenye sifa na uzoefu stahiki kwa biashara ya Takaful.</p> <p>(b) Atalazimika kuteua Afisa Matekelezo wa Shariah kwa kuendana na matakwa ya Mwongozo huu.</p> <p>(c) Atahakikisha kuwa Takaful ya Familia inagawanywa katika mifuko ya ziada ikiwemo Mifuko ya Takaful ya washiriki, Mifuko ya Uwekezaji ya Washiriki na mingineyo kama itakavyoelekezwa na Bodi ya Shariah kwa ushauri wa Mtakwimu bima.</p> <p>(d) Anaeendesha biashara ya Takaful ya kawaida, atapaswa kuanzisha</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<p>(e) Shall ensure that all investments made in any Participant Takaful Fund are approved by its Shariah Board</p> <p>(f) Shall ensure that assets and liabilities of each Participant Takaful Fund and Participant Investment Fund are segregated from its other assets and liabilities;</p> <p>(g) Shall ensure that receipts and payments from Participant Takaful Fund are made in accordance with the provisions of these guidelines</p> <p>(h) Shall ensure that the Participant Takaful Fund, at all times, carry reserves in accordance with the provisions of these guidelines;</p> <p>(i) Shall ensure that there is in each Participant Takaful Fund a surplus of</p>		<p>mfuko mmoja au zaidi wa washiriki wa Takaful na mfuko wa Muendeshaji.</p> <p>(e) Atahakikisha kuwa uwekezaji uliofanywa na Mfuko wowote wa Washiriki unaidhinishwa na Bodi ya Shariah.</p> <p>(f) Atahakikisha kuwa mali na madeni ya kila Mfuko wa Washiriki wa Takaful na Mfuko wa uwekezaji wa Washiriki vinatenganishwa na mali zake zingine na madeni.</p> <p>(g) Atahakikisha kuwa mapato na malipo yoyote kutoka kwenye mfuko wa Takaful wa Washiriki yanafanyika kwa mujibu wa maelekezo ya Mwongozo huu.</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<p>admissible assets over liabilities in accordance with the provisions of these guideline</p> <p>(j) Shall manage the Participant Takaful Fund and related risks in accordance with the provisions of these guidelines;</p> <p>(k) Where admissible assets in a Participant Takaful Fund are not sufficient to cover liabilities, the deficit shall be funded by way of an interest-free loan in accordance with the provisions of these guidelines;</p> <p>(l) Shall determine the quantum of surplus or deficit in each Participant Takaful Fund in accordance with the provisions of these guidelines;</p> <p>(m) Shall set the fee structure and the profit-sharing ratio for investment</p>		<p>(h) Atahakikisha kuwa Mfuko wa Takaful wa Washiriki, wakati wote utakuwa na akiba kwa mujibu wa matakwa ya Mwongozo huu.</p> <p>(i) Atahakikisha kuwa katika kila Mfuko wa Takaful wa Washiriki kutakuwa na ziada ya mali zinazokubalika dhidi ya madeni kwa mujibu wa matakwa ya Mwongozo huu.</p> <p>(j) Atasimamia Mfuko wa Takaful wa Washiriki pamoja na majanga yanayohusiana nayo kwa mujibu wa matakwa ya Mwongozo huu.</p> <p>(k) Endapo mali zinazokubalika katika Mfuko wa Takaful wa Washiriki hazitoshelezi kukidhi madeni, nakisi itagharamiwa na mkopo</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	management between the Takaful operator and Takaful participants in accordance with the provisions of these guidelines in accordance with the advice of the Shariah board and the appointed actuary and approved by the Commissioner of Insurance.		<p>usiokuwa na riba kwa mujibu wa matakwa ya Mwongozo huu.</p> <p>(l) Atalazimika kutathmini kiwango cha ziada au nakisi katika kila Mfuko wa Takaful wa Washiriki kwa mujibu wa matakwa ya Mwongozo huu.</p> <p>(m) Atalazimika kuweka muundo wa ada na uwiano wa kugawana faida kwa ajili ya usimamizi wa uwekezaji baina ya Muendesha na Washiriki wa Takaful kwa kuzingatia ushauri wa Bodi ya Shariah na Mtakwimu Bima na kuidhinishwa na Kamishna.</p>
2.3 Takaful Intermediaries	2.3.1 Registration requirements for insurance brokers and agents as provided for in the Insurance Act Cap	2.3 Mawakala (Watu wa	2.3.1 Masharti ya Kusajiliwa kwa madalali na mawakala wa bima kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	394 will be applicable to Takaful intermediaries	kati wa Takaful	Bima Sura Na. 394 pia yatatumika kwa mawakala wa kati wa Takaful.
2.3.2	Where a broker conducts both Takaful and conventional insurance business, the broker shall be required to maintain a separate account for each business and ensure that the funds in the trust account of the Takaful business are maintained in a Shari'ah compliant bank.		2.3.2 Ikiwa dalali anajihusisha na Takaful na pia bima ya kawaida, dalali huyo atatakiwa kutenganisha akaunti za fedha za amana za kila biashara na kuhakikisha kuwa fedha zilizoko katika akaunti ya amana ya Biashara ya Takaful zinawekwa katika benki zinazoendana na misingi ya Sheriah.
2.3.3	Each Takaful business registrant shall attend Takaful training from time to time as may be determined by the Authority;		2.3.3 Kila msajiliwa wa bima ya Takaful atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya Takaful mara kwa mara kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.
2.3.4	Takaful registrants are required to have and abide by necessary controls to reduce possibility of miss-selling, and shall fulfill the following:		2.3.4 Msajiliwa wa Takaful atapaswa kuweka vidhibiti kuzuia udanganyifu na atatekeleza yafuatayo:

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	<p>(a) Attend training on applicable Takaful guidelines;</p> <p>(b) Attend product training prior to commencing the business.</p> <p>2.3.5 Takaful registrants shall promote products and services in a manner that is clear, fair and not misleading, while maintaining Shari'ah rules and principles at all times.</p>		<p>(a) Kuhudhuria mafunzo kuhusu Miongozo ya Takaful</p> <p>(b) Kuhudhuria mafunzo juu ya bidhaa kabla ya kuanza biashara</p> <p>2.3.5 Wasajiliwa wa Takaful watazitungaza bidhaa na huduma kwa mfumo ulio wazi, wenye haki na usiopotosha pamoja na kukidhi matakwa ya kanuni za Shariah na misingi yake kwa wakati wote.</p>
<p>2.4 Registration and Licening</p>	<p>2.4.1 Takaful business shall be registerd and licensed to operate in Tanzania when the business:</p> <p>(a) Meets registration requirements as prescribed by the the Insurance Act Cap 394 and Takaful guidelines 2022.</p> <p>(b) The License is non-transferable.</p>	<p>2.4 Usajili na Leseni</p>	<p>2.4.1 Biashara ya Takaful itasajiliwa na kupata leseni ya kuendesha shughuli zake nchini Tanzania ikiwa:</p> <p>(a) Itakidhi masharti kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Bima Sura Na. 394 na Mwongozo wa Takaful 2022</p> <p>(b) Leseni haitohamishika</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
	(c) Takaful business licensed by the Authority shall carry out related activities in accordance with these Guidelines and within the terms and conditions of the issued license.		(c) Biashara ya Takaful yenye leseni ya Mamlaka itaendesha shughuli zake kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa katika leseni
2.5 Cancellation/Suspension of Registration	<p>2.5.1 In addition to the provisions on cancelation of registration listed in the Insurance Act Cap 394; the Commissioner may cancel registration of Takaful business where he is satisfied that:</p> <p>(a) A Takaful Operator willfully violates Shariah compliance or Shariah governance as determined by the Shariah board.</p> <p>(b) Takaful Operator halts its Takaful operations without the permission of the Authority</p>	2.5 Kufuta/Kusitisha kwa Muda Usajili	<p>2.5.1 Pamoja na matakwa ya kisheria yaliyoainishwa katika Sheria ya Bima Sura Na. 394, Kamishna anaweza kufuta Usajili wa Biashara ya Takaful ikiwa atajiridhisha kuwa:</p> <p>(a) Muendesha Takaful kwa makusudi anakiuka matakwa ya Shariah au usimamizi bora wa Shariah kama ilivyowekwa na Bodi ya Shariah.</p> <p>(b) Endapo Muendesha Takaful atasitisha uendeshaji biashara ya Takaful bila idhini ya Mamlaka</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS	SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA
<p>(c) The Takaful operator has failed to maintain minimum admissible assets and liabilities requirements;</p> <p>(d) The operator has ceased to carry on Takaful business in respect of any class of Takaful business without prior approval of the Commissioner.</p> <p>(e) The operator has failed to comply with solvency requirements</p> <p>(f) The operator is carrying on its Takaful business in a manner likely to be detrimental to the interests of its participants;</p> <p>(g) It is in the public interest to cancel the registration</p> <p>(h) The operator has failed to effect satisfactory Re-Takaful arrangements.</p>	<p>(c) Ikiwa Muendesha biashara ya Takaful ameshindwa kudumisha kiwango cha chini cha mali na madeni kinachohitajika.</p> <p>(d) Muendesha biashara ya Takaful amekoma kuendelea na Biashara katika kundi lolote la Biashara ya Takaful bila kupata idhini ya Kamishna.</p> <p>(e) Muendesha biashara ya Takaful ameshindwa kukidhi masharti ya ukwasi.</p> <p>(f) Muendesha anaendesha Biashara ya Takaful kwa mwenendo wenye muelekeo wa kuhatarisha maslahi ya Washiriki.</p> <p>(g) Ikiwa kufuta Usajili kuna maslahi ya umma.</p> <p>(h) Muendesha ameshindwa kuweka utaratibu mzuri wa Takaful mtawanyo</p>

SECTION TWO: POLICY REQUIREMENTS		SEHEMU YA PILI: MASHARTI YA MKATABA	
2.6 Winding Up of Takaful Business	<p>2.6.1 Winding up of Takaful Business is required to fully comply with the provisions of the Insurance Act Cap 394 and the requirements listed below:</p> <p>(a) The assets of a Takaful fund shall be applied to meet the liabilities to Takaful funds</p> <p>(b) Assets comprised in the deposit made by a Takaful operator in respect of either class of business may be allocated by the Commissioner to any Takaful fund established by the Takaful operator for that class of business in such manner and proportion as he sees fit, and assets so allocated shall be treated as assets of the Takaful fund</p>	2.6 Kufunga Biashara ya Takaful	<p>2.6.1 Ili kufunga biashara ya Takaful inahitajika kukidhi kwa ukamilifu matakwa ya Sheria ya Bima Sura Na. 394 na matakwa yaliyoorodheshwa hapa chini:</p> <p>(a) Mali za Mfuko wa Takaful zitatumika kulipia dhima ya mfuko wa Washiriki wa Takaful</p> <p>(b) Mali ambazo ni sehemu ya amana iliyowekwa na Muendesha Takaful kuhusiana na kundi lolote la Takaful linaweza kuhamishwa kwenda kwenye mfuko wowote wa Takaful ulioanzishwa na Muendesha Takaful kwa ajili ya kundi hilo kwa utaratibu na kiwango ambacho Kamishna ataona inafaa na amana hizo zitachukuliwa kuwa ni mali za mfuko huo.</p>

SECTION THREE: ESTABLISHMENT AND MAINTENANCE OF TAKAFUL FUNDS		SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL	
<p>3.1 Establishment and Maintenance of Takaful Funds</p>	<p>3.1.1 A Takaful operator must establish general Takaful funds or family Takaful funds separate from its Shareholders fund. These funds accumulate all or portion of participants' contributions that are pooled to fulfill any claims arising from eligible claimants within the cover period. Under a Tabarru' (donation) contract the fund is collectively owned by the pool of participants.</p> <p>3.1.2 An Operator shall, for each Participants Risk Fund, formulate Participant Takaful Fund Policies defining:</p> <p>(a) Risks being covered;</p>	<p>3.1 Uanzishaji na Uendelezaji wa Mifuko ya Takaful</p>	<p>3.1.1 Muendesha biashara ya Takaful ataanzisha mfuko wa Takaful ya kawaida au ya familia tofauti na mfuko wa wanahisa. Mifuko hii itatunza sehemu au michango yote ya wachangiaji inayokusanywa kwa ajili ya madai halali ndani ya kipindi cha kinga. Katika mkataba wa Tabarru, Mfuko unamilikiwa kwa pamoja na washiriki.</p> <p>3.1.2 Kwa kila Mfuko wa majanga wa Washiriki, Muendeshaji ataunda utaratibu, Sera za Mfuko wa washiriki wa Takaful akiainisha:</p> <p>(a) Majanga yatakayofidiwa;</p> <p>(b) Matukio ambayo yatasababisha kulipwa viwango stahiki kutoka katika</p>

SECTION THREE: ESTABLISHMENT AND MAINTENANCE OF TAKAFUL FUNDS	SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL
<p>(b) The events upon which amounts would be payable from the Participants Risk Fund to a participant and the method of determination of the amount payable;</p> <p>(c) Expenses which may be charged to the Participants Risk Fund;</p> <p>(d) The method and frequency of determining surpluses or deficits of the Participants Risk Fund, including a definition of how any reserves being set aside in determining such surpluses or deficits are to be arrived at;</p> <p>(e) The method of distribution of any surplus;</p> <p>(f) The method of extinguishing any deficit; and</p>	<p>mfuko wa washiriki na namna viwango hivyo vitakavyoamuliwa kulipwa kutoka katika Mfuko wa majanga wa Washiriki kwenda kwa mshiriki;</p> <p>(c) Gharama zinazoweza kutozwa kutoka katika Mfuko wa Majanga wa Washiriki;</p> <p>(d) Namna na mara ngapi watatathmini ziada au nakisi katika mfuko wa majanga wa washiriki, ikiwepo kwa namna gani ziada au nakisi zitakokotolewa;</p> <p>(e) Namna ya kugawana ziada;</p> <p>(f) Namna ya kuondoa nakisi yeyote; na</p> <p>(g) Utaratibu wa kuvunja Mfuko wa Majanga wa Washiriki.</p>

SECTION THREE: ESTABLISHMENT AND MAINTENANCE OF TAKAFUL FUNDS		SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL	
	(g) The procedure for dissolution of Participants Risk Fund.		
3.2 Participants Risk Fund	<p>3.2.1 Takaful Operator may create a single Participants Risk Fund or several Participants Risk Funds for different classes of businesses:</p> <p>(a) A participants' risk fund shall be a separate fund, the purpose of which shall be the pooling of funds of the participants.</p> <p>(b) The role of the Takaful operator shall be the management of the participants' risk funds and related risks.</p> <p>(c) At the initial stages of the set-up of participants' risk funds; the Takaful operator and any of its shareholders may at their discretion make an initial</p>	3.2 Mfuko wa Majanga wa Washiriki	<p>3.2.1 Muendesha Takaful anaweza kuunda Mfuko mmoja wa Washiriki au mifuko kadhaa kwa makundi tofauti ya biashara:</p> <p>(a) Mfuko wa majanga wa Washiriki utakuwa ni mfuko wa kipekee wenye lengo la kujumuisha michango ya washiriki.</p> <p>(b) Wajibu wa Muendesha Takaful utakuwa ni kusimamia mifuko ya majanga ya washiriki na majanga husika.</p> <p>(c) Katika hatua za awali za kuunda mifuko ya majanga ya washiriki, Muendesha Takaful na wanahisa wake, kwa hiari yao, wanaweza kutoa mchango au</p>

SECTION THREE: ESTABLISHMENT AND MAINTENANCE OF TAKAFUL FUNDS	SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL
<p>donation or Benevolent loan (Qardh Hasana) to the participants' risk funds.</p> <p>(d) The objectives of participants' risk funds shall be to provide relief to participants against defined losses.</p> <p>(e) The Takaful operator shall define participants' risk funds' rules which shall be in accordance with the generally accepted principles and norms of insurance business with guidance by the Shari'ah board of the Takaful operator.</p> <p>(f) Any subsequent changes to the participants' risk funds' rules shall also be approved by the Shariah board.</p>	<p><i>Mkopo wa hisani (Qardh Hasana)</i> katika mifuko ya majanga ya washiriki.</p> <p>(d) Malengo ya mifuko ya majanga ya washiriki yatakuwa kuwapa unafuu washiriki dhidi ya hasara zilizoainishwa.</p> <p>(e) Muendesha Takaful atainisha kanuni ambazo zitaendana na misingi na desturi zinazokubalika katika tasnia ya bima ambazo zitaendana na mwongozo wa Bodi ya Shariah ya Muendesha Takaful.</p> <p>(f) Mabadiliko yoyote ya kanuni za mifuko ya majanga ya washiriki yatakayojitokeza yatalizimika kuidhinishwa na Bodi ya Shariah.</p>

SECTION THREE: ESTABLISHMENT AND MAINTENANCE OF TAKAFUL FUNDS		SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL	
3.3 Inflow of Participants Risk Fund	<p>3.3.1 Inflows to the Takaful Risk Fund shall consist of:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Contributions from participants to the Takaful Risk Fund; (b) Notwithstanding the provisions of (a) above, for the case of a Family Takaful Operator, contributions to the Takaful Risk Fund net of any amounts credited directly to Participants Investment Funds or the Operator sub-fund; (c) Share of claims from Re-Takaful; (d) Investment income generated by the investment of funds retained in the Participant Risk Fund; (e) Salvages and Recoveries in the case of General Takaful; (f) Benevolent loan (Qardh Hasana); 	3.3 Maduhuli ya Mfuko wa Majanga ya Washiriki	<p>3.3.1 Maduhuli ya Mfuko wa Majanga wa Takaful yatajumuisha:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Michango kutoka kwa washiriki kwenda kwenye mfuko wa Majanga ya Washiriki; (b) Bila kuathiri maudhui ya kifungu (a) hapo juu, kwa Takaful ya Familia, mfuko wa majanga utaundwa na salio baada ya makato yote yaliyolipwa kwenye Mfuko wa Uwekezaji wa Washiriki au Mfuko mdogo wa Muendeshaji; (c) Sehemu ya fidia inayolipwa na Takaful Mtawanyo; (d) Mapato yatokanayo na uwekezaji wa michango iliyopo kwenye Mfuko wa Majanga wa Washiriki; (e) Masalio na Marejesho ikiwa inahusu Takaful za kawaida;

SECTION THREE: ESTABLISHMENT AND MAINTENANCE OF TAKAFUL FUNDS		SEHEMU YA TATU: UANZISHAJI NA UENDELEZAJI WA MIFUKO YA TAKAFUL	
	<p>(g) Commission from Re-Takaful operators;</p> <p>(h) Share of surplus from Re-Takaful operators;</p> <p>(i) Donation made by the shareholders of the Takaful operator.</p>		<p>(f) Mkopo wa Hisani (Qardh Hasana);</p> <p>(g) Malipo kutoka kwa Waendesha Takaful Mtawanyo;</p> <p>(h) Sehemu ya ziada kutoka kwa waendeshaji wa Takaful Mtawanyo;</p> <p>(i) Msaada uliotolewa na wanahisa wa Muendesha Takaful.</p>
	11.1.3 The contract between Takaful Operator and Participant shall be made where an offer by the Takaful Operator is accepted by the participant by signing it and the required contribution is paid.		11.1.3 Mkataba baina ya Muendesha Takaful na Mshiriki utakua umeingiwa pale ambapo pendekezo la Muendesha Takaful limekubaliwa na Mshiriki kwa kuweka sahihi yake na kulipa mchango stahiki.
	11.1.4 The Takaful Operator shall issue a Takaful Certificate to evidence the existence of the contract.		11.1.4 Muendesha Takaful atatoa Hati ya Takaful kwa mshiriki ili kuthibitisha kuwepo kwa mkataba

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
12.1 Takaful Operating Models	<p>12.1.1 Takaful operations categorized into two types/classes as follows:</p> <p>(a) Family Takaful is typically a long-term arrangement between the Takaful Operator and Takaful participant providing financial relief.</p> <p>(b) General Takaful is typically a short-term agreement between the Takaful Operator and Takaful participant providing financial compensation for specified losses.</p>	12.1 Miundo ya Uendeshaji wa Takaful	<p>12.1.1 Shughuli za Takaful zimegawanyika katika makundi mawili kama ifuatavyo:</p> <p>(a) Takaful ya Familia, ni mpangilio wa bima ya muda mrefu kati ya Muendesha Takaful na Mshiriki wa Takaful kumpatia msaada wa kifedha.</p> <p>(b) Takaful ya Kawaida, ni makubaliano ya muda mfupi kati ya Muendesha Takaful na Mshiriki wa Takaful kutoa fidia ya kifedha kwa hasara maalum.</p>
12.2 Adoption of Operating Model	<p>12.2.1 The Takaful operator is required to adopt an operating model which shall have been approved by the Board of directors and the Shariah board</p> <p>12.2.2 Takaful participant and Takaful Operator enter a contractual</p>	12.2 Kupitishwa kwa Muundo wa Uendeshaji	<p>12.2.1 Muendesha Takaful atalazimika kuwa na muundo wa uendeshaji ambao utakuwa umeidhinishwa na Bodi ya Shariah na Bodi ya Wakurugenzi.</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS	SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL
<p>relationship for Takaful services for a fee. The Takaful Operator will establish and document one of the following operating models to conduct Takaful business:</p> <p>(a) Takaful based on Mudharabah (Profit sharing) Contract In this model, the Takaful Operator holds the role of the Mudarrib (Entrepreneurial Partner) and the Takaful Participants are the Rabul-mal (owner of capital). The key aspects of the model are set out in the contract and shall include:</p> <p>(i) Takaful Operator manages investment and underwriting activities.</p>	<p>12.2.2 Mshiriki wa Takaful na Muendesha Takaful wanaingia kwenye uhusiano wa kimkataba wa huduma za Takaful kwa ada. Muendesha Takaful ataanzisha na kuweka katika maandishi mojawapo ya miundo ya uendeshaji ifuatayo ili kufanya biashara ya Takaful:</p> <p>(a) Takaful kulingana na Mkataba wa Mudharabah (kugawana faida). Katika muundo huu, Muendesha Takaful anakuwa Mudarrib (Msimamizi wa mtaji) na Washiriki wa Takaful ni Rabul-mal (mmiliki wa mtaji). Vipengele muhimu vya muundo huu vitaainishwa katika mkataba na kujumuisha mambo yafuatayo:</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS	SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL
<p>(ii) The percentage share of investments gains between the Takaful Operator and Participants.</p> <p>(iii) Financial losses to be borne by Takaful participants.</p> <p>(b) Takaful based on Wakalah (Agency)</p> <p>In this model, the Takaful Operator holds the role of the Wakil (the agent) acting on behalf of the Takaful Participants in return for a fee. The key aspects of the model are set out in the contract and will include:</p> <p>(i) Takaful Operator manages investment and underwriting activities.</p> <p>(ii) Takaful Operator for performing this service will receive a Wakalah (Agency) fee that is set out in the contract.</p>	<p>(i) Muendesha Takaful atasimamia uwekezaji na shughuli za uandishi wa bima.</p> <p>(ii) Asilimia ya faida ya uwekezaji itakayogawanywa baina ya Muendesha Takaful na Mshiriki wa Takaful.</p> <p>(iii) Hasara ya uwekezaji itabebwa na Washiriki wa Takaful</p> <p>(b) Muundo wa Takaful wa Uwakalah</p> <p>Katika Muundo huu Muendesha Takaful ni Wakalah anaefanya kazi kwa niaba ya Washiriki kwa malipo ya ada. Mambo ya msingi katika muundo huu yanatakiwa yaainishwe katika mkataba na yatajumuishwa:</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS	SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL
<p>(iii) Takaful Operator is also permitted to receive a performance related fee as per the contract.</p> <p>(c) Takaful based on Hybrid Wakalah-Mudharabah (Agency - Profit sharing) contract</p> <p>In this model, a Wakalah (Agency) contract is in place between the Takaful Operator and the Takaful participants for the management of underwriting activities and a Mudharabah (Profit sharing) contract is between the Takaful Operator and the Takaful participants for the investment activities.</p> <p>(d) Waqf Model</p> <p>Takaful Operator creates a Waqf Fund where participants contribute their contributions on the basis of “Tabarru” into this Waqf Fund.</p>	<p>(i) Muendesha Takaful atasimamia uwekezaji na shughuli za uandishi wa bima.</p> <p>(ii) Muendesha Takaful atalipwa ada ya Uwakalah kama itakavyo bainishwa katika mkataba wake.</p> <p>(iii) Muendesha Takaful anaruhusiwa pia kupokea ada inayotokana na utendaji kazi mzuri kulingana na mkataba</p> <p>(c) Takaful kulingana na muundo jumuishi wa Wakalah-Mudharabah (Wakalah-kugawana faida),</p> <p>Katika muundo huu, kuna mkataba wa uwakalah baina ya Muendesha Takaful na Washiriki wa Takaful katika usimamizi wa uandishi wa bima. Na mkataba wa</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS	SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL
<p>The relationship of the participants with the Waqf fund is such that the Takaful Operator is the Wakeel (Agent) of the participants in the management of the Fund.</p> <p>The Waqf fund shall work to achieve the following objectives:</p> <ul style="list-style-type: none"> (i) To extend financial assistance to the participants in the event of losses. (ii) To extend benefits to the participants strictly in accordance with the Waqf Deed. <p>Hybrid of the Waqf model and either Wakala or Mudharabah models can also be adopted as approved by the Shari'ah Board</p> <p>12.2.3 Takaful Operator shall obtain prior written approval from the Authority before launching or amending any model.</p>	<p>Mudharabah (kugawana faida) baina ya Muendesha Takaful na Washiriki wa Takaful katika shughuli za uwekezaji.</p> <p>(d) Muundo wa Wakfu</p> <p>Muendesha Takaful ataunda Mfuko wa Wakfu ambapo washiriki watachangia michango yao kwa msingi wa "Tabarru" katika Mfuko huu wa Wakfu.</p> <p>Uhusiano wa washiriki wa mfuko wa wakfu ni kwamba Muendesha Takaful ni wakalah wa washiriki katika usimamizi wa mfuko.</p> <p>Mfuko wa Wakfu utafanya kazi ili kufikia malengo yafuatayo;</p> <ul style="list-style-type: none"> (i) Kutoa msaada wa kifedha kwa washiriki wake wakati wa tukio la hasara; (ii) Kutoa fidia kwa washiriki wake kwa kuzingatia makubaliano ya Wakfu.

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	12.2.4 The Takaful Operator shall disclose the operating model(s) adopted for use within the participants' policy documentation and its annual report.		<p>Mseto wa muundo wa Wakfu na muundo wa Wakalah au Mudharabah utaweza kutumika kama itakavyoidhinishwa na Bodi ya Shariah.</p> <p>12.2.3 Muendesha Takaful atapata idhini ya maandishi kutoka kwenye Mamlaka kabla ya kuzindua au kurekebisha muundo wowote.</p> <p>12.2.4 Muendesha Takaful ataweka wazi muundo au miundo aliyochagua kutumika katika mkataba wake na Washiriki na katika taarifa ya mwaka.</p>
12.3 The Account for the Family Takaful	<p>12.3.1 The contributions in the Family Takaful arrangement shall be divided into two accounts:</p> <p>(a) Participants Investment Account: is an account to which a portion of</p>	12.3 Akaunti ya Takaful ya Familia	<p>12.3.1 Michango katika Takaful ya Familia itagawanywa katika akaunti mbili;</p> <p>(a) Akaunti ya Uwekezaji wa Washiriki: ni akaunti ambayo sehemu ya michango iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	<p>contributions allocated for investment in this type of Takaful shall be transferred. Provided that in determining the suitable distribution ratios for the funds the operator shall abide by the opinion of the actuary.</p> <p>(b) Participants Special Account: is an account to which a portion of contributions allocated for risk coverage in this type of Takaful shall be transferred.</p>		<p>itawekwa. Isipokuwa kwamba katika kuamua uwiano unaofaa wa mgawanyo wa fedha Muendesha atatii maoni ya Mtakwimu.</p> <p>(b) Akaunti Maalum ya Washiriki: ni akaunti ambayo sehemu ya michango iliyotengwa kwa ajili ya kinga ya majanga katika aina hii ya Takaful itawekwa.</p>
<p>12.4 Remuneration for the Management of Takaful Funds</p>	<p>12.4.1 A Takaful operator may be remunerated in consideration for the services rendered, costs incurred and performance outcome in managing Takaful funds. Any such remuneration may include elements of fixed remuneration (i.e., upfront</p>	<p>12.4 Malipo ya Usimamizi wa Fedha za Takaful</p>	<p>12.4.1 Muendesha Takaful anaweza kulipwa kwa kuzingatia huduma zinazotolewa, gharama zinazotumika na matokeo ya utendaji katika kusimamia fedha za Takaful. Ujira wowote mwingine unaweza kujumuisha vipengele vya</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	<p>Wakalah (agency fee), performance-based remuneration and compensation for direct costs incurred.</p> <p>12.4.2 Takaful Operator's fee shall cover the total sum of the following components:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Management expenses. (b) Distribution expenses including intermediary's remuneration and agents' commission. (c) Other expenses involved in making Takaful products available to the public. (d) A reasonable appropriate margin of operational profits in case of occurrence of a surplus in Takaful fund. 		<p>malipo yasiyobadilika yaani ada ya wakala, malipo yanayotegemea ufanisi wa usimamizi na fidia kwa gharama za moja kwa moja zinazotumika</p> <p>12.4.2 Ada ya Muendesha Takaful itagharamia jumla ya vipengele vifuatavyo;</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Gharama za usimamizi; (b) Gharama za usambazaji ikijumuisha malipo ya Watu wa kati na ujira wa Mawakala; (c) Gharama zingine zinazohusika katika upatikanaji wa bidhaa za Takaful kwa umma; (d) Kiwango stahiki cha faida ya uendeshaji iwapo ziada itatokea katika Mfuko wa Takaful.

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	<p>12.4.3 A Takaful operator must establish and implement remuneration guidelines which ensure that –</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) The remuneration structure reflects the specific work or services undertaken; (b) The remuneration is consistent with prudent risk-taking, preserves the interest of the Takaful participants and ensures the long-term sustainability of the Takaful funds. <p>12.4.4 Where the Takaful Operator remuneration includes amounts based on the surplus in the Participants’ Risk Fund, the following conditions must be met:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) There must be no interest free loan balance due to the 		<p>12.4.3 Muendesha Takaful atatengeneza na kutekeleza Mwongozo wa malipo ambayo inahakikisha kwamba -</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Muundo wa ujira unaonyesha kazi au huduma mahususi zilizofanywa; (b) Malipo yanalingana na uzito wa majanga kwa busara, kulinda maslahi ya Washiriki wa Takaful na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa mfuko wa Takaful. <p>12.4.4 Pale ambapo malipo kwa Muendesha Takaful yanahusu ziada katika Mfuko wa majanga kwa Washiriki, masharti yafuatayo lazima yazingatiwe:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Lisiwepo salio la mkopo usio na riba kutokana na fedha za Wanahisa za Muendesha Takaful;

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	<p>Shareholders funds of the Takaful- Operator;</p> <p>(b) The remuneration must be in line with the Takaful Operators Surplus Management Procedures and subject to review of an actuary. (Schedule 3: Takaful Operating Policy; Part 12)</p> <p>(c) Remuneration to Takaful Operator is only permitted if Participants will also be receiving their share of the surplus;</p> <p>(d) Total remuneration payable to the Takaful Operator shall not exceed surplus to be received by the participants.</p>		<p>(b) Malipo lazima yalingane na Taratibu za Usimamizi wa Ziada ya Waendeshaji Takaful na kutegemeana na maoni ya Mtakwimu bima. (Kiambatisho Na. 3: Sera ya Uendeshaji wa Takaful; Sehemu ya 12)</p> <p>(c) Malipo kwa Muendesha Takaful yataruhusiwa endapo tu Washiriki watakuwa wamepokea sehemu yao ya ziada;</p> <p>(d) Jumla ya malipo yanayolipwa kwa Muendesha Takaful hayatazidi ziada itakayopokelewa na Washiriki.</p> <p>12.4.5 Pale ambapo malipo ya Muendesha Takaful yanajumuisha kiasi kulingana na faida ya uwekezaji kutoka kwa Mfuko wa Uwekezaji wa</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	<p>12.4.5 Where the Takaful Operator's remuneration includes amounts based on the investment profit from the Participants Investment Fund, the following conditions shall be considered</p> <p>(a) Investment profit to be calculated in line with the Takaful Operators policy.</p> <p>(b) Investment net profit distribution based on independently audited results of the Participant Risk Fund with Actuarial certification of the liabilities.</p> <p>(c) Distribution to be recommended by the actuary and endorsed by the Shariah board and approved by the Board of Directors of the Takaful Operator.</p>		<p>Washiriki, masharti yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa.</p> <p>(a) Faida ya uwekezaji itakokotolewa kwa mujibu wa sera za Waendesha Takaful;</p> <p>(b) Ugawaji wa faida safi ya uwekezaji kulingana na matokeo ya ukaguzi wa mahesabu unaojitegemea pamoja na uthibitishaji wa Mtakwimu bima;</p> <p>(c) Mgawanyo utapendekezwa na Mtakwimu, kupendekezwa na Bodi ya Shariah na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Muendesha Takaful;</p> <p>(d) Mgawanyo wa faida ya uwekezaji utaendana na uwiano wa ugavi wa</p>

SECTION TWELVE: TAKAFUL OPERATING MODELS		SEHEMU YA KUMI NA MBILI: MIUNDO YA UENDESHAJI WA TAKAFUL	
	<p>(d) Distribution of the investment profit to be in line with the profit-sharing ratio set out in the Takaful contract.</p> <p>(e) Distribution does not impact solvency of the fund.</p>		<p>faida uliowekwa katika Mkatiba wa Takaful;</p> <p>(e) Ugawaji hauathiri ukwasi wa mfuko.</p>
<p>12.5 Performance Fee-Added</p>	<p>A Takaful operator shall develop a procedures related to calculation of Performance fee that shall be endorsed by the Shariah Board and Approved by the Board of directors (Schedule 3: Takaful Operating Policy; Part 13)</p>	<p>12.5 Ada ya Ufanisi</p>	<p>Muendesha Takaful ataweka taratibu kuhusiana na namna ya kukokotoa ada ya ufanisi ambayo itapitishwa na Bodi ya Shariah na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi. (Kiambatisho Na. 3: Sera ya Uendeshaji wa Takaful; Sehemu ya 13)</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
13.1 Takaful Governance	13.1.1 Takaful business shall only be operated when it is established as a limited liability company or a subsidiary of an insurance company and has complied with relevant registration and licensing requirements stipulated in the Insurance Act Cap 394 and relevant specific requirements prescribed in these Guidelines.	13.1 Utaratibu wa Usimamizi wa Takaful	13.1.1 Biashara ya Takaful haitafanyika isipokua pale ambapo imeanzishwa kama kampuni yenye ukomo wa dhima au kampuni tanzu ya kampuni ya bima na kukidhi masharti ya usajili kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya bima Sura Na. 394 pamoja na masharti mahususi yaliyowekwa kwenye Mwongozo huu.
	13.1.2 Takaful operator shall provide information to the Authority on their Shariah governance framework for the purpose of ensuring Shariah compliance in their entire Takaful business activities.		13.1.2 Muendesha Takaful atatoa taarifa kwa Mamlaka kuhusu utaratibu wa usimamizi wa Shariah kwa madhumuni ya kuhakikisha uzingatiaji wa Shariah katika shughuli zao zote za biashara ya Takaful.
13.2 Shariah Board	13.2.1 Takaful Operator shall not commence its operation unless it has	13.2 Bodi ya Shariah	13.2.1 Muendesha Takaful kabla ya kuanza shughuli zake anatakiwa kuunda Bodi

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	<p>in place a Shariah Board duly appointed to ensure the operations are in line with Shariah principles.</p> <p>(a) The Shariah board members shall be approved by the company's board of directors;</p> <p>(b) Shariah Board shall consist of minimum of three members;</p> <p>(c) The Shariah scholars should always hold a majority of the Shariah board membership;</p> <p>(d) The members shall elect one of them as the chairman;</p> <p>(e) The Shariah board membership term shall be three years renewable.</p> <p>13.2.2 Takaful operator shall facilitate Continuous trainings of the Shariah board members.</p>		<p>ya Shariah ili kuhakikisha shughuli za Takaful zinafata misingi ya Shariah.</p> <p>(a) Wajumbe wa bodi ya Shariah watapitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni;</p> <p>(b) Bodi ya Shariah itakuwa na wajumbe wasiopungua watatu;</p> <p>(c) Wanazuoni wa Shariah daima wanapaswa kushikilia wingi wa wajumbe wa Bodi ya Shariah;</p> <p>(d) Wanachama watamchagua mmoja wao kuwa mwenyekiti;</p> <p>(e) Muda wa uanachama wa bodi ya Shariah utakuwa miaka mitatu inayoweza kuongezwa.</p> <p>13.2.2 Muendesha Takaful atawezesha mafunzo endelevu kwa wajumbe wa Bodi ya Shariah.</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
<p>13.3 Minimum Qualifications of Shariah Board Members</p>	<p>13.3.1 Takaful Operator shall ensure that every member of the Shariah Board fulfills the following criteria:</p> <p>(a) To be Fit and Proper;</p> <p>(b) Shall be Muslim, enjoying the legal capacity;</p> <p>(c) Must be at least a diploma holder of Shariah or Islamic Finance studies from a registered institution;</p> <p>(d) Not a shareholder, a member of the board of directors, or employee of the Takaful operator or any other Takaful operator in Tanzania.</p>	<p>13.3 Sifa na vigezo vya Wajumbe wa Bodi ya Shariah</p>	<p>13.3.1 Muendesha Takaful atahakikisha kwamba kila mjumbe wa Bodi ya Shariah anatimiza sifa na vigezo vifuatavyo</p> <p>(a) Mwenye sifa zinazotakiwa;</p> <p>(b) Awe Muislam mwenye sifa zinazokidhi haja;</p> <p>(c) Lazima awe angalau mwenye diploma ya Shariah au elimu ya mfumo ya fedha ya Kiislamu kutoka kwa taasisi iliyosajiliwa;</p> <p>(d) Asiwe mwanahisa, mjumbe wa bodi ya wakurugenzi, au mwajiriwa wa Muendesha Takaful au Muendesha mwingine yeyote wa Takaful nchini Tanzania.</p>
<p>13.4 Circumstances where the Authority</p>	<p>13.4.1 Authority may refuse appointment or terminate an appointment of individual from Shariah board membership where the individual:</p>	<p>13.4 Mazingira ambayo Mamlaka Inaweza kukataa Uanacha</p>	<p>13.4.1 Mamlaka inaweza kukataa uteuzi au kuzuia uteuzi wa mtu binafsi kuwa mjumbe wa bodi ya Shariah pale ambapo mtu huyo:</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
may Refuse Shariah Board Membership	<p>(a) Does not meet the fit and proper requirements;</p> <p>(b) Is declared bankrupt or a petition under bankruptcy laws is filed against him;</p> <p>(c) Is found guilty with any serious criminal offence or any other offence punishable with imprisonment of one year or more.</p>	ma wa Bodi ya Shariah	<p>(a) Hakidhi vigezo na sifa zinazotakiwa;</p> <p>(b) Ametangazwa kuwa amefilisika au maombi chini ya sheria ya ufilisi yamewasilishwa dhidi yake;</p> <p>(c) Anapatikana na hatia kwa kosa lolote kubwa la jinai au kosa lingine lolote ambalo adhabu yake ni kifungo cha mwaka mmoja au zaidi.</p>
13.5 Functions of Shariah Board	Takaful Operator shall be responsible to lay out duties and functions of the Shariah Board in line with best practices.	13.5 Majukumu ya Bodi za Shariah	Muendesha Takaful atawajibika kuinisha majukumu na kazi za Bodi ya Shariah kwa kuzingatia misingi ya utendaji bora.
13.6 Authority of the Shariah Board	<p>13.6.1 All Shariah board resolutions shall be final and binding to the Takaful Operator.</p> <p>13.6.2 The Shariah board shall have the right to access, at any time, all</p>	13.6 Mamlaka ya Bodi ya Shariah	<p>13.6.1 Maazimio yote ya bodi ya Shariah yatakuwa ya mwisho na Muendesha Takaful atalazimika kuyatekeleza.</p> <p>13.6.2 Bodi ya Shariah itakuwa na haki ya kuzipata, wakati wowote, rekodi zote za</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	<p>Takaful Operator's records, contracts, and documents; and may require clarifications as it deems necessary to perform its tasks.</p> <p>13.6.3 The Takaful Operator's management shall provide such clarifications.</p>		<p>Muendesha Takaful, mikataba na nyaraka; na inaweza kuhitaji ufafanuzi itakapona ni muhimu ili kutekeleza majukumu yake.</p> <p>13.6.3 Menejimenti ya Muendesha Takaful italazimika kutoa ufafanuzi huo.</p>
<p>13.7 Public Access to Shariah Board</p>	<p>13.7.1 The Takaful Operator shall ensure that the list of Shariah board members are made available to the public.</p> <p>13.7.2 The Shariah Board certificate for each product being offered by the Takaful Operator, shall be made public.</p>	<p>13.7 Ufikiaji wa Shariah Bodi na Umma</p>	<p>13.7.1 Muendesha Takaful atahakikisha kwamba orodha ya Wajumbe wa Bodi ya Shariah inawekwa wazi na wanajulikana kwa umma.</p> <p>13.7.2 Muendesha Takaful ataweka wazi kwa umma Cheti cha Bodi ya Shariah kilichoidhinisha kila bidhaa anayotoa.</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
<p>13.8 Duties and Responsibilities of the Takaful Operator Towards Shari’ah Board</p>	<p>13.8.1 The Takaful Operator shall ensure:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) All contracts and products are referred to the Shariah board. (b) The Shariah Board’s recommendations and decisions are implemented and issued to stakeholders appropriately. (c) All Takaful products are certified by the Shariah Board before being offered to the market. (d) The Report of the Shariah Board is published within its annual financial report. (e) Standard operating procedure of the Shariah Board is in place. (f) The Shariah Board has access to all the relevant records, transactions or other information 	<p>13.8 Wajibu na majukumu ya Muendesha Takaful kwa Bodi ya Shariah</p>	<p>13.8.1 Muendesha Takaful atahakikisha:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Mikataba yote na bidhaa zote vitawasilishwa katika Bodi ya Shariah. (b) Mapendekezo na maamuzi ya Bodi ya Shariah yanatekelezwa na taarifa kutolewa kwa wadau ipasavyo. (c) Bidhaa zote za Takaful zithibitishwe na Bodi ya Shariah kabla ya kupelekwa sokoni. (d) Taarifa ya Bodi ya Shariah ichapishwe pamoja na taarifa ya fedha ya mwaka. (e) Utaratibu wa kawaida wa uendeshaji wa Bodi ya Shariah umeandaliwa. (f) Bodi ya Shariah inakuwa na uwezo wa kupata taarifa zote husika, miamala ya Takaful au taarifa

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	<p>required for the performance of its duties.</p> <p>(g) The Shariah Board has sufficient resources to perform its duties.</p> <p>(h) Appropriate level of remuneration for members of the Shariah Board commensurate with the expected duties and functions</p>		<p>nyingine zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.</p> <p>(g) Bodi ya Shariah ina rasilimali za kutosha kutekeleza majukumu yake.</p> <p>(h) Kiwango kinachostahiki cha malipo kwa wajumbe wa Bodi ya Shariah kinalingana na majukumu na kazi zinazotarajiwa.</p>
13.9 Principal Officer Qualifications	<p>13.9.1 Every Takaful operator shall employ a full-time principal officer who shall be;</p> <p>(a) A holder of a degree in Islamic finance or insurance with diploma in Takaful or certified Shariah Advisor/Auditor from recognized and reputable institution;</p>	13.9 Sifa za Afisa Mkuu	<p>13.9.1 Kila Muendesha Takaful ataajiri Afisa Mkuu ambaye atawajibika kwa utendaji wa siku hadi siku wa shughuli za Takaful katika kampuni ambaye atakuwa na sifa zifuatazo;</p> <p>(a) Mwenye shahada ya fedha ya Kiislamu au mwenye shahada ya bima pamoja na diploma ya Takaful au Mshauri/Mkaguzi wa Shariah aliyeidhinishwa kutoka</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	<p>(b) A person with a good command of Kiswahili or English language; and</p> <p>(c) A person with at least three years post qualification experience in financial sector at managerial level</p> <p>13.9.2 Appointment of the principal officer shall require prior approval of the Commissioner.</p>		<p>taasisi inayotambulika na inayoheshimika;</p> <p>(b) Mtu mwenye ujuzi mzuri wa lugha ya Kiswahili au Kiingereza; na</p> <p>(c) Mtu mwenye uzoefu wa angalau miaka mitatu baada ya kufuzu katika sekta ya fedha katika ngazi ya usimamizi.</p> <p>13.9.2 Uteuzi wa Afisa Mkuu utahitaji idhini ya Kamishna kabla ya kuanza utumishi wake</p>
13.10 Shariah Compliance Officer	<p>13.10.1 Takaful Operator shall have a Shariah compliance officer</p> <p>13.10.2 Shariah Compliance Officer shall have sufficient knowledge of Islamic jurisprudence</p> <p>13.10.3 Shariah Compliance Officer shall serve as a link between the</p>	13.10 Afisa Utekelezaji wa Shariah	<p>13.10.1 Muendesha Takaful lazima awe na Afisa Utekelezaji wa Shariah</p> <p>13.10.2 Afisa Utekelezaji wa Shariah atakuwa na ujuzi wa kutosha wa Sheria za Kiislamu</p> <p>13.10.3 Afisa wa Utekelezaji wa Shariah atahudumu kama kiungo kati ya Bodi ya</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	<p>Shariah Board and management of the Takaful Operator.</p> <p>13.10.4 Shariah Compliance Officer shall serve as secretary of the Shariah board.</p>		<p>Shariah na Menejimenti ya Muendesha Takaful.</p> <p>13.10.4 Afisa Utekelezaji wa Shariah atahudumu kama katibu wa Bodi ya Shariah</p>
<p>13.11 Qualification of Shariah Compliance Officer</p>	<p>13.11.1 A University Degree in Islamic Law or Islamic Studies majoring in Banking and Finance or Business Administration or Economics or its equivalent from a recognized institution. OR</p> <p>13.11.2 A Diploma in Islamic Law or Islamic Studies majoring in Banking and Finance or Business Administration or its equivalent from a recognized institution.</p>	<p>13.11 Sifa za Afisa Utekelezaji wa Shariah</p>	<p>13.11.1 Shahada ya Chuo Kikuu katika Sheria ya Kiislamu au Mafunzo ya Kiislamu yenye taaluma ya Benki na Fedha au Utawala wa Biashara au Uchumi au inayolingana nayo kutoka katika taasisi inayotambulika. AU</p> <p>13.11.2 Diploma ya Sheria ya Kiislamu au Mafunzo ya Kiislamu yenye taaluma ya Benki na Fedha au Utawala wa Biashara au inayolingana nayo kutoka katika taasisi inayotambulika</p> <p>13.11.3 Uzoefu wa miaka mitatu (3) katika taasisi ya kifedha inayotoa huduma za</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	13.11.3 Three (3) year's Islamic finance experience in a similar role from a reputable organization.		kifedha za Kiislamu inayotambulika kisheria.
13.12 External Shariah Auditor	<p>13.12.1 A Takaful operator shall appoint a Takaful Shariah external auditor, recognised by Islamic finance profession accrediting institutions and approved by the Commissioner.</p> <p>13.12.2 Shariah auditor shall conduct Shariah audit of the Takaful Operator for each accounting period and issue report.</p>	13.12 Mkaguzi wa Nje wa Shariah	<p>13.12.1 Muendesha Takaful atateua Mkaguzi wa Nje wa Shariah, anayetambuliwa na taasisi zinazoidhinisha taaluma ya fedha ya Kiislamu na kuidhinishwa na Kamishna.</p> <p>13.12.2 Mkaguzi wa Shariah atafanya ukaguzi wa Shariah kwa Muendesha Takaful kwa kila kipindi cha mahesabu na kutoa taarifa.</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE	SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL
<p>13.12.3 For the purpose of these guidelines, the Shariah audit shall cover all aspects of the Takaful business operations and activities in accordance with the requirements of the Companies' Act or recognised International Shariah, Accounting, Auditing, or Governance standards.</p> <p>13.12.4 The audit work shall include but not limited to obtaining assurance that:</p> <p>a. The Takaful Operator has separated the assets of the Participants Risk Fund(s) and the Takaful operator fund with appropriate checks and balances in place to ensure the funds cannot be integrated;</p>	<p>13.12.3 Kwa madhumuni ya Mwongozo huu, ukaguzi wa Shariah utashughulikia vipengele vyote vya shughuli za biashara ya Takaful kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni au viwango vinavyotambulika vya Shariah, Uhasibu, Ukaguzi au Usimamizi wa Kimataifa.</p> <p>13.12.4 Pamoja na mambo mengine, Kazi ya ukaguzi itajumuisha kuhakikisha kwamba:</p> <p>a. Muendesha Takaful ametenganisha mali za Mfuko wa majanga wa Washiriki na mali za Muendesha Takaful na kuhakikisha mali hazichanganywi katika mfuko mmoja;</p> <p>b. Muendesha Takaful ametenganisha Mifuko ya Majanga ya Washiriki na Mfuko wa Uwekezaji wa Washiriki;</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE	SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL
<ul style="list-style-type: none"> b. The Takaful Operator has separated the Participants Risk Fund and Participants Investment Fund; c. The Takaful operator is remunerated in line with the Takaful model adopted and the amounts determined in underlying contracts; d. Management expenses are paid from the Takaful Operators shareholders' funds; e. Expenses paid out of Takaful funds are claims and related expenses or direct investment related expenses that have been approved by the Shariah Board; f. That investment activity performed by the Takaful Operator is in compliance with Shariah; 	<ul style="list-style-type: none"> c. Muendesha Takaful analipwa kulingana na aina ya muundo wa uendeshaji wa Takaful uliopitishwa na kiasi kilichoamuliwa katika mikataba ya msingi; d. Gharama za uendeshaji zinalipwa kutoka kwenye Mfuko wa wanahisa wa Muendesha Takaful; e. Gharama zinazolipwa kutoka kwenye Mfuko wa Takaful ni madai ya Takaful na gharama zitokanazo na madai au gharama zinazohusiana na uwekezaji ambazo zimeidhinishwa na Bodi ya Shariah; f. Shughuli za uwekezaji zinazofanywa na Muendesha Takaful zinazingatia Kanuni za Kishariah; g. Muendesha Takaful amebainisha na kukokotoa mapato yasiyoruhusiwa na kutolewa ipasavyo;

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	<p>g. The Takaful operator has appropriately identified, calculated and disbursed impermissible income.</p> <p>13.12.5 Obtaining assurance that any surplus generated in the Participants Risk Fund is managed in line with the policy approved by the Shariah Board</p> <p>13.12.6 Obtaining assurance that any deficit in the Participants Risk Fund or Participants Investment Fund is appropriately managed in compliance with Shariah and the Takaful Operator documented policies.</p> <p>13.12.7 Shariah Auditor shall submit a report on Shariah audit to Shariah Board and Takaful Operator.</p> <p>13.12.8 Takaful Operator shall prepare a plan for correcting the</p>		<p>13.12.5 Kuhakikisha kwamba ziada yoyote inayotokana na Mfuko wa Majanga wa Washiriki wa Takaful inasimamiwa kwa mujibu wa sera iliyoidhinishwa na Bodi ya Shariah</p> <p>13.12.6 Kuhakikisha kwamba nakisi yeyote katika Mfuko wa Majanga wa Washiriki au Mfuko wa Uwekezaji wa Washiriki unasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa Shariah na sera zilizowekwa na Muendesha Takaful</p> <p>13.12.7 Mkaguzi wa Shariah atawasilisha taarifa ya ukaguzi wa Shariah kwa Bodi ya Shariah na Bodi ya Wakurugenzi.</p>

SECTION THIRTEEN: TAKAFUL GOVERNANCE		SEHEMU YA KUMI NA TATU: USIMAMIZI WA TAKAFUL	
	findings of Shariah audit report and submit it to Shariah Board and implement its corrective action plan		13.12.8 Muendesha Takaful ataandaa mpango wa kutekeleza taarifa ya ukaguzi wa Shariah na kuiwasilisha kwenye bodi ya Shariah na kutekeleza mpango huo.
13.13 Rating of a Takaful Operator	A Takaful operator is required to be rated by a Shariah compliance rating agency licensed by TIRA and its rating report submitted to the Authority.	13.13 Tathmini ya Muendesha Takaful	Muendesha Takaful atatakiwa kutathminiwa na wakala wa Utathmini aliyesajiliwa na Mamlaka na taarifa za tathmini zitawasilishwa kwenye Mamlaka.

SECTION FOURTEEN: RE-TAKAFUL		SEHEMU YA KUMI NA NNE: TAKAFUL MTAWANYO	
<p>14.1 Re-Takaful</p>	<p>14.1.1 A Takaful Operator may obtain re-Takaful services from a locally licensed or accredited foreign Re-Takaful Operator as per the Insurance Act.</p> <p>14.1.2 In case Re-Takaful is not feasible, the Shariah Board may give an exceptional approval for the use of conventional Re-insurance.</p>	<p>14.1 Takaful Mtawanyo</p>	<p>14.1.1 Muendesha Takaful anaweza kupata huduma za Takaful mtawanyo kutoka kwa Muendesha Takaful mtawanyo wa ndani mwenye leseni au wa nje aliye pewa ithibati na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria za Bima</p> <p>14.1.2 Ikiwa Muendesha Takaful mtawanyo hatopatikana, Bodi ya Shariah inaweza kutoa idhini ya dharura kutumia bima mtawanyo ya kawaida.</p>

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
15.1 Accounting Guidelines	Takaful Operator shall prepare its accounts in observance of the Minimum requirements provided under schedule One to these Guidelines.	15.1 Mwongozo wa Kihasisibu	Muendesha Takaful atatarisha hesabu zake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Mwongozo huu.
15.2 Benevolent Loan (Qardh Hasana)	Benevolent Loan payable by the Takaful Operator is part of the financial obligations of the Operator to the Takaful Risk Fund.	15.2 Mkopo wa Hisani (Qardh Hasana)	Mkopo wa Hisani unaotolewa na Muendesha Takaful kwenda kwenye Mfuko wa Majanga wa Washiriki wa Takaful ni sehemu ya wajibu wa kifedha wa Muendesha Takaful kwa Mfuko wa majanga ya washiriki
15.3 Disclosure on Benevolent Loan	15.3.1 The Takaful operator shall disclose in the annual financial statements in relation to any issued benevolent loan, the following: (a) The circumstances which necessitated the Takaful operator to provide benevolent loan to the Takaful Risk fund from its shareholders' fund;	15.3 Uwekaji wazi wa Mkopo wa Hisani	15.3.1 Muendesha Takaful atabainisha katika taarifa fedha za mwaka yafuatayo kuhusiana na mkopo wowote wa hisani uliotolewa: (a) Mazingira yaliyosababisha Muendesha Takaful kutoa Mkopo wa hisani kwa mfuko wa majanga wa washiriki.

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
	(b) Evidence of an unsuccessful attempt to call upon other available options leading to benevolent loan as Last Resort to solve the illiquidity of the Participants Risk Fund.		(b) Ushahidi wa kujaribu bila mafanikio kutumia njia nyingine hivyo kusababisha kutoa mkopo wa hisani kama hatua ya mwisho kutatua tatizo la ukwasi katika Mfuko wa majanga wa Washiriki.
15.4 Repayment of Benevolent Loan	<p>15.4.1 Takaful Operator shall disclose accounting measurement to be applied in respect to the application of time value for money to determine the present and future value of benevolent loan including any fair value adjustment.</p> <p>15.4.2 Shareholders shall have a right to recover the actual advanced benevolent loan from the Takaful Risk Fund without any increment.</p>	15.4 Marejesho ya Mkopo wa Hisani (Qardh Hassan)	<p>15.4.1 Muendesha Takaful atatakiwa kutoa ufafanuzi kuhusiana na matumizi ya thamani ya fedha kutegemeana na muda ili kupata thamani ya mkopo wa hisani kwa wakati uliopo na ujao pamoja na marekebisho yoyote ya thamani yaliyo ya haki.</p> <p>15.4.2 Wanahisa watakuwa na haki ya kurejeshewa mkopo wa hisani waliutoa kwa Mfuko wa Majanga wa Washiriki bila ongezeko lolote</p>

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
15.5 Conditions for Issuance of Benevolent Loan	<p>15.5.1 The Takaful Operator may issue Benevolent loan to the Participants Fund subject to the following conditions; -</p> <p>(a) As the Last Resort to solve the illiquidity of the Participants Risk Fund following an unsuccessful attempt to call upon other available options;</p> <p>(b) If a special Actuarial Valuation has been carried out to establish the causative reason(s) of the deficit in the Takaful Risk Fund.</p>	15.5 Masharti ya Utoaji wa Mkopo wa Hisani	<p>15.5.1 Muendesha Takaful anaweza kutoa mkopo wa hisani kwa Mfuko wa Washiriki kwa masharati yafuatayo; -</p> <p>(a) Ikiwa ni hatua ya mwisho ya kutatua tatizo la nakisi katika Mfuko wa Majanga wa Washiriki baada ya kujaribu bila mafanikio njia mbadala zilizopo;</p> <p>(b) Iwapo tathmini maalum ya kitakwimu bima kubainisha sababu ya kutokea nakisi katika Mfuko wa Majanga wa Washiriki wa Takaful imefanyika.</p>
15.6 Measures for misappropriation of Takaful Risk Fund	<p>15.6.1 The Commissioner may, in addition to the measures provided under the Insurance Act Cap 394, take the following measures against any Takaful operator who misappropriates, miss-manages or</p>	15.6 Hatua za Matumizi mabaya ya Mfuko wa	<p>15.6.1 Kamishna anaweza kuchukua hatua zifuatazo pamoja na nyingine zilizopo kwenye Sheria ya Bima Sura Na. 394, dhidi ya Muendesha Takaful yeyote ambaye amefuja, ameshindwa kusimamia kwa weledi au kusababisha</p>

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
	<p>otherwise causes deficit in the Takaful Risk Fund:</p> <p>(a) Require the Takaful operator to pay from his own sources an amount equivalent to the occasioned deficit;</p> <p>(b) Where the deficit to the Participants Fund is not by any means blamable to the Takaful Operator, then the Takaful Operator will advance a benevolent loan to the Participants Fund to be repaid when the Participants Fund has realized surplus and in accordance with the policy on extinguishing deficits in the Participants Fund.</p>	<p>Majanga ya Washiriki</p>	<p>nakisi katika Mfuko wa Majanga wa Takaful:</p> <p>(a) Kumtaka Muendesha Takaful kulipa kutoka vyanzo vyake mwenyewe kiasi sawa na nakisi aliyosababisha;</p> <p>(b) Ikiwa imethibitishwa kuwa nakisi haikutokana na Muendesha Takaful, hivyo basi Muendesha takaful atatoa Mkopo wa Hisani ili kujaziliza nakisi, utakaolipwa wakati ambapo Mfuko wa Washiriki utakapokuwa na ziada na kulingana sera ya kuondoa nakisi katika Mfuko wa Washiriki.</p>

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
<p>15.7 The Published Financial Statements</p>	<p>15.7.1 The following are the provisions applicable to Published Financial Statements:</p> <p>(a) The accounting requirements stipulated under the Act shall apply to Takaful business with appropriate modifications based on the advice of the Shariah Board prior to approval by the Commissioner;</p> <p>(b) The published financial statements shall consist of the following statements:</p> <ul style="list-style-type: none"> (i) Statement of financial position; (ii) Statement of comprehensive income; (iii) Statement of cash flows; (iv) Statement of changes in shareholders' equity and Takaful Participants Fund; and 	<p>15.7 Taarifa za Kifedha Zilizochapishwa</p>	<p>15.7.1 Masharti yafuatayo yatatumika kwa ajili ya Taarifa za Kifedha zilizochapishwa;</p> <p>(a) Masharti ya uhasibu yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bima yatatumika kwa biashara ya Takaful baada ya marekebisho yanayofaa kuzingatia ushauri wa Bodi ya Shariah na kuidhinishwa na Kamishna.</p> <p>(b) Taarifa za kifedha zilizochapishwa zitakuwa kama ifuatavyo:</p> <ul style="list-style-type: none"> (i) Taarifa ya hali ya kifedha; (ii) Taarifa ya mapato kamili; (iii) Taarifa ya mtiririko wa fedha; (iv) Taarifa ya mabadiliko katika fedha za wanahisa na Mfuko wa Washiriki wa Takaful; na (v) Maelezo ya taarifa za kifedha.

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
	<p>(v) notes to the financial statements</p> <p>15.7.2 The Operator shall prepare statement of financial position with a combined statement of comprehensive income of Participants Risk Fund(s) and Shareholders' Fund while showing the two separately</p> <p>15.7.3 In line with the international best standards, the Operator shall submit to the commissioner accounts and balance-sheet together with a certificate signed by an auditor.</p>		<p>15.7.2 Muendesha Takaful ataandaa taarifa ya hali ya kifedha inayojumuisha mapato kamili ya Mfuko wa Majanga wa Washiriki na fedha za Wanahisa kuonesha taarifa hizo tofauti.</p> <p>15.7.3 Kwa kuzingatia viwango bora vya kimataifa, Muendesha Takaful atawasilisha kwa Kamishna hesabu na mizania pamoja na cheti kilichosainiwa na Mkaguzi wa Hesabu.</p>

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
15.8 Notes to the Financial Statements	<p>15.8.1 The explanatory notes to be disclosed in the annual financial statements shall include the following information:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) A description on the role of Takaful operator; (b) Any forms of remuneration paid to the Takaful operator; (c) The amount of surplus distribution, if any, to both Takaful participants and shareholders' fund; (d) Any other forms of financial support received by the Takaful Risk Fund from the shareholders' fund (e) Any gift provided as additional Takaful benefits payable from the shareholders' fund to the Takaful 	15.8 Maelezo kwa Taarifa za Kifedha	<p>15.8.1 Maelezo yatakayobainishwa katika taarifa za fedha za mwaka yatajumuisha Maelezo kuhusu:</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) Majukumu ya Muendesha Takaful; (b) Malipo yoyote yanayolipwa kwa Muendesha Takaful; (c) Kiasi cha mgao wa ziada, kama kitakuwepo, kwa Mfuko wa Washiriki wa Takaful na Wanahisa; (d) Aina nyingine yeyote ya msaada wa kifedha uliopokelewa na Mfuko wa Majanga wa Takaful kutoka kwa fedha za Wanahisa. (e) Zawadi yoyote iliyotolewa kwa Mfuko wa Washiriki kutoka kwenye Mfuko wa Wanahisa kama nyongeza ya maslahi ya kawaida;

SECTION FIFTEEN: ACCOUNTING GUIDELINES		SEHEMU YA KUMI NA TANO: MWONGOZO YA KIHASIBU	
